OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA
SHULE YA SEKONDARI CHIROMBOLA
S.L.P 17
MAHENGE/ULANGA

JINA LA MWANAFUNZI.....

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHIROMBOLA ILIYOPO WILAYA YA ULANGA MKOA WA MOROGORO MWAKA .....

1.0. UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba, umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Chirombola **HONGERA SANA.** Ni matumaini yetu kuwa wewe mzazi/mlezi utashirikiana na uongozi wa shule katika malezi ili mwanao aweze kuitumia nafasi hii adimu kwa manufaa yake na taifa kwa ujumla.
Muhura wa masomo utaanza tarehe ..... Ili kuwezesha usajili kufanyika kikamilifu, mwanao anashauriwa kufika shuleni siku hiyo na kuripoti ofisi ya mkuu wa shule.

2.0 MAHITAJI MUHUMU NA VIFAA VYA SHULE

Napenda kukujulisha kuwa mwanao ajapo shuleni anahitajika kuja na

2.1 SARE SAHIHI ZA SHULE AMBAZO NI:

- Suruali mbili (2) kwa wavulana na sketi mbili (2) kwa wasichana za kitambaa cha kijani kibichi zilizoshonwa kwa heshima, isiyobana, yenye mifuko, isiyo kama ya jinsi. Aidha sketi iwe ya marinda inayovuka magoti na suruali iwe nap indo na marinda.(akivaa modo au suluali ya kubana au fupi hatapokelewa).
- T-shirt ya Bluu yenye nembo ya shule,
- Mashati meupe mawili (2) yasiydangaza
- Viatu vya ngozi rangi nyeusi vya kamba, buti, yebo yebo na viatu vya kuchomeka haviruhusiwi kabisa.
- Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana
- Mkanda wa suluali rangi nyeusi usio na urembo
- Tai na sweta rangi ya kijani
- Kwa watoto wa kike wa kiislam wanapaswa kuvaa Hijab au kuvaa blauzi nusu kanzu.

2.2 SALE ZA MICHEZO

- Raba pea moja (1)
- Trak-suti moja (1) rangi ya blue yenye mistari myeupe.

2.3 VIFAA VYA DARASANI

- Mzazi unashauriwa kumnunulia mwanao daftari zenye gamba gumu, yaani counter book zinazoweza kudumu kwa muda mrefu na zisizopungua kumi (10)
- Kalamu za wino za bluu na nyeusi za kutosha, penseli, mkebe na rula.
- Kamusi ya awali Oxford-ndogo (kingereza kwa kiswahili) kwa ajili ya kumsaidia mwanafunzi kujifunza lugha ya kingereza.
- File moja la kuhifadhia kumbukumbu za mwanafunzi.
- Bagi dogo la kubebea vifaa vya mwanafunzi na mkebe mmoja (mathematical set)

2.5 LISHE

- Mzazi unatakiwa uhakikishe mwanao anapata chakula cha mchana shuleni kwa kufuata taratibu zilizowekwa katika vikao vya wazazi kwa kushirikiana na viongozi wa kamati ya chakula ya wazazi.

AFYA

Chukua fomu iliyoambatishwa na fomu ya maelekezo na ipeleke kwa mganga wa kituo cha afya /zahanati inayotambuliwa na serikali ili mwanafunzi afanyiwe uchunguzi wa afya ili shule ipate kufahamu matatizo yake maalumu kama vile; damu, macho masikio n.k

3.0 (a) SHERIA

4.0 NA KANUNI MBALIMBALI ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa na sheria ya elimu Na. 10 ya mwaka 1995.

Aidha shule hii inazingatia miongozo yote iliyotolewa na wizara ya elimu yenye dhamana ya utoaji elimu nchini na ofisi ya Rais TAMISEMI yenye dhamana ya usimamizi wa elimu, mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo anapokuja kusajiliwa na kuwa mwanafunzi wa shule hii.

a) Kuwa na heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzie na jamii kwa ujumla.
b) Maudhurio mazuri shuleni kila siku bila kukosa isipokuwa kwa ruhusa maalumu
c) Kuwahi shuleni na kushiriki katika shughuli zote za shule kikamilifu
d) Kutunza haiba yake kwa usafi wa mwili, lugha na mavazi.
e) Kutunza mali za shule wakati wote.
f) Kuvaa sale za shule wakati wote isipokuwa kwa ruhusa au shughuli maalumu.
g) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo au kutokuwepo eneo la shule.
h) Kupokea na kuwaelekeza wageni kutokana na mahitaji yao mbalimbali wafikapo shuleni.
i) Kujiepusha na kibuli, hasira na kutoa kauli chochezi, lugha za matuzi na zinazoweza kuudhi.

(b) MAELEZO MENGINE YA KINIDHAMU

Kila mwanafuzni afikapo shuleni atapewa sheria za shule ambazo atahitajika kuzifuata hata hivyo makosa yafuatayo yanaweza kumfukuzisha mwanafunzi shule akiyafanya.

i. Wizi.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii. Kugoma au kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzako, walimu, walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yoyote yule.
vi. Kufuga ndevu.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevywa.
viii. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
ix. Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yanayovunja sheria za nchi.
x. Uvutaji wa sigara, kusababisha au kumpa mimba msichana.
xi. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xiii. Kudharau bendera ya Taifa.
xiv. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
xv. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

Mwisho!

"Nakukaribisha shule ya sekondari chirombola" Karibu sana na hongera sana ufikapo ripoti ofisi ya mkuu wa shule.

KARIBU SANA CHIROMBOLA SEKONDARI

.....

MKUU WA SHULE
CHIROMBOLA SEKONDARI

MKUU WA SHULE
CHIROMBOLA SEC. SCHOOL
S.L.P. 11 MAHENGE
MOROGORO